# Gazeti la Kimataifa

**Waabuduo Damu ya Kristo**

ASC Mawasiliano ya Kimataifa – Uongozi Mkuu - Via Maria De Mattias, 10 - 00183 Roma

www.adoratrici-asc.org redazioneasc@adoratrici-asc.org

...Kwa Neno Lako...

Lima, Peru
5-28 Luglio 2017

Mwaka XXIII – 18 Mei 2021


## Siku maalum ya tarehe 18 Mei 2021

hafla ya maadhimisho ya miaka 18 **ya utakatifu Maria De Mattias**

## Taarifa ya Tarehe 18 Mei

*"Sherehekea ya kumbukumbu ya kutangazwa kwa Mtakatifu Maria De Mattias ambaye Utakatifu wake unatuwezesha kutafakari juu ya wito wetu wa kuabudu na utume wetu. Tuwe tayari kuangazwa na kutiwa moyo kwa mfano wake kama mwanafunzi anayependwa na Kristo Bwana ambaye ni mfano wa upendo wa kishujaa kwa wanadamu wote."*

Sr. Nadia Coppa, ASC
Barua ya mwaliko wa adhimisho

Tarehe hii 18 Mei 2021 hakika ilikuwa siku ya kukumbukwa. Kwa kweli, kwenye hafla ya maadhimisho ya miaka 18 ya utakatifu Maria De Mattias, Sr. Nadia alitoa wazo la kuadhimisha Ekaristi Takatifu kwa Waabudu 20 ambao kuanzia 2020 walianza kutuacha baada ya kuambukizwa maambukizi ya COVID-19.

Katika jumuiya ambazo walikuwepo Masista hawa kumekuwa na mateso mengi, kwa sababu ya kutengwa, ukosefu wa msaada wa kiroho, na kutopata nafasi ya kuwasaidia Masista wagonjwa na kutowezekana kwa kuwaaga kwa mazishi stahiki. Kila kitu kimekuwa uzoefu wa Fumbo la Pasaka ambalo limetuunganisha Shirika zima.

Hivyo lilitolewa wazo la kuadhimisha on line kupitia jukwaa la ZOOM. Uongozi ulipokea pendekezo hilo kwa hisia za kushangaza na shauku.

Kwa hivyo, siku iliyosubiriwa ilikuja kati ya hofu ya maandalizi na furaha ya kuweza kukutana na Masista wengi kutoka Mashariki hadi Magharibi, kutoka Kaskazini hadi Kusini mwa Shirika. Shukrani hizi zote zote ziwafikie wale wote waliotafsiri.

## Muhtasari


- Taarifa ya tarehe 18 Mei 1

*Ujumbe kutoka kwa Mkuu wa Shirika*
- Ukaribisho – Sr Nadia Coppa 3

*Toka Ulimwengu wa ASC*
- Bwana Yesu, Unajifanya chakula na kinywaji kwa ajili yetu, ukituwekea Roho wako wa Kimungu ndani mwetu. - *Italia* 5
- Mimi, shahidi wa upendo wa ASC - *Italia* 6
- Tafakari ya tarehe 18 Mei - *Italia* 6
- Kumfuata Maria De Mattias - *Polonia* 7

Mwangwi wa Sherehe
- *- Schaan* 8
- *- Zagabria* 9
- Shukrani - *Tanzania* 11
- Mrejesho wa sherehe - *US* 12
- "Upendo usio na mipaka" - *India* 15

*Hitimisho la Mkuu wa Shirika*
- Shukrani– Sr Nadia Coppa 17

*Katika Shirika*
- Maadhimisho ya Vifo vya ASC vilivyotokana na COVID 19


Sherehe hiyo ilifanyika chini ya bendera ya kimataifa: La celebrazione si è svolta all'insegna dell'internazionalità: Maandamano ya kuingia yalisindikizwa na wimbo wa Mtakatifu Maria De Mattias kwa Kiswahili, masomo yalisomwa kwa Kiitaliano na Kiingereza, Sala za waumini zilitolewa kwa lugha mbali mbali za wanashirika; matoleo yalisindikizwa na wimbo wa kicroato, dossologia ilikuwa ni kwa Ki-Malaialam, na mwisho baada ya maneno ya shukrani ya Sr Nadia, adhimisho la Misa lilimalizika kwa kuimba wimbo wa Mtakatifu Maria De Mattias mbele ya kaburi lake.

Baada ya mahubiri ya Mwadhama Kardinali Joao Braz de Aviz, Mkuu wa CIVCSVA ambaye aliongoza adhimisho hilo, tuliwakumbuka Masista marehemu waliokufa kwa Covid, tukiwashukuru kwa zawadi ya maisha yao, na ishara ndogo ya kawaida iliyoturuhusu kuonyesha upendo wetu na shukrani zetu kwa yale ambayo wameyafanya kwa ajili yetu. Tukiwaita kwa majina, tulitoa taa, ishara ya maisha yao kama waabudu, iliyoangazwa na Kristo Bwana, katika nyayo za Mtakatifu Maria De Mattias; "Kama vile mabikira wenye busara wa Injili ambayo Bwana aliwakuta tayari kuingia kwenye harusi ya milele pamoja naye, wanaweza kuimba utukufu wa mwana-kondoo", yalikuwa maoni ya utangulizi ambayo yalifuatana na wakati huo.

Wamisionari wa CPPS, Mapadri wa parokia mbili za parokia za karibu, kuzaliwa kwa Yesu na Mtakatifu Catherine wa Siena, na mapadre wa Rosminian walituheshimu kwa uwepo wao. Jumuiya 187 kutoka kote ulimwenguni zilisajiliwa mkondoni.

Jioni ilimalizika kwa muda wa agape ya kindugu.

***Sr Maria Grazia Boccamazzo, ASC***



## Ujumbe wa ukaribisho kutoka kwa Mkuu wa Shirika

*Asubuhi njema, mchana mwema na jioni njema!*

*Nawasalimu kwa Upendo Masista wote mlioungana pamoja nasi katika adhimisho hili kutoka Ulimwenguni kote, kuanzia Australia mpaka Argentina. Na hii ni hafla muhimu ambayo inatufanya tuonane pamoja leo katika ukumbusho wa maadhimisho ya kumi na nane ya Utakatifu wa Maria De Mattias. Tunawakaribisha kwa Upendo ninyi nyote mliopo hapa na salamu ya pekee kwa Mh Kardinali Joao Braz de Aviz – Mkuu wa Taasisi za Masirika ya Kitawa na jamii za maisha ya Kitume ambaye alipokea kwa furaha mwaliko wa adhimisho hili la Ekaristi.*

*Nawashukuru ndugu zetu waliopo hapa, Mapadri ambao wameamua kuungana nasi kwa namna ya pekee na yenye maana kwa tukio hili.*



Imepita miaka 18 tangu ile tarehe 18 Mei ya 2003. Sisi sote tuna kumbukumbu nzuri mioyoni mwetu katika uwanja wa Mtakatifu Petro uliojazwa na kofia nyekundu ambazo ziliandikwa: Thamani yako ni Damu ya Kristo!

Leo katika wakati huu ambao hauna uhakika mwingi bado kunabaki ndani yetu na karibu nasi, kama wakati huo, tunatakiwa kuwa tayari kuangazwa na kutiwa moyo na mfano wa mpendwa wetu Maria De Mattias, dada, rafiki, mama, mwanzilishi, aliyeishi maisha yake kwa ukamilifu wa kitume, uliotofautishwa na Upendo usio na masharti, kwa Mungu na kwa wanadamu wote.

Covid katika mwaka huu imetushtua sote na kutufanya tuwe katika hali ya kujiandaa. Dhamana zetu nyingi zimejaribiwa sana, hadi maisha yetu. Tulipitia usiku wa giza kweli, usiku wa moyo, "usiku mweusi". Janga hili bado linaendelea kutupatia changamoto, na kuonyesha udhaifu mwingi: kibinafsi, kijumuiya, na kwenye taasisi. Na sisi pia, kama Shirika, tumekuwa na wakati wa maumivu makubwa. Na bado tuna hofu kubwa. Ninafikiria Region ya India, Masista wa Brazil, ambao hali yao ni ngumu sana. Machungu yasiyokuwa ya kawaida. Uzoefu chungu wa shida ya kiafya isiyokuwa ya kawaida.

Virusi hivi vimewaondoa wapendwa wetu: maisha ya marafiki, Masista wetu. Kama mwizi vimetuibia sehemu yetu kwa kuingia kwa nguvu maishani mwetu, nyumba zetu, undugu wetu kwa namna, inayoweza kuthubutu kusema, kuleta maumivu mengi. Tumepata mateso mengi kila mahali kama Shirika.

Masista kadhaa walituacha bila hata kutupa nafasi ya kuwaaga. Upweke, kutengwa, ugumu hata wa kusema kwa heri.

Hata hivyo ninaamini kuwa uwepo wa maumivu haya yote katika jumuiya zetu umetumika kuthibitisha mwamko mpya: kuishi kwetu kama "mahujaji" njiani. Tuko njiani kuelekea nyumbani. Akiwa njiani kwenda nyumbani kwa Baba akiwa amemkazia Yesu macho, au kama vile Maria De Mattias atakavyosema : juu ya mpendwa aliye Juu zaidi.

Hatua kwa hatua, kwa neema, hata kwa moyo uliovuja damu, tulitoka kwa hisia za hasira, huzuni, hadi kukubali ukweli wa hali halisi tofauti. Tulizoea kusoma wakati huu katika Pasaka ya Yesu na kuzingatia kile kilicho muhimu: maisha bila mwisho.

Wakati huu wa wasiwasi, ulikuwa kama miamba juu ya moyo. Nyuso mara nyingi zilitokwa na machozi, maneno matupu, hayakutosha mbele ya maumivu mengi. Wakati mgumu kuuelezea na kuwa ni Nuru tu ya imani inayoweza kuangaza. Ninaamini kwamba hizi zilikuwa siku ambazo, zaidi ya wakati mwingine, tuliishi kitambulisho chetu kama Waabuduo Damu ya Kristo. Iliyotambulishwa na Fumbo la Pasaka kwamba, kwa undani, tumeitwa kuishi Karama yetu, tumejitolea kwa ujasiri kwa Baba. Na Bwana, ambaye anajua kusudi la vitu vyote, ametusaidia kuishi wakati huu kwa njia ya ukombozi, kutuwezesha kutabiri siku mpya ambayo anataka kutupatia.

# Ujumbe kutoka kwa Mkuu wa Shirika



Kwa hiyo tupo hapa sote kwa pamoja, kama mwili mmoja kukiri ukweli huu: tunaweza kugeuza maombolezo kuwa kukiri kwa imani. Tunaweza kutangaza kweli kwamba kifo ni matunda ikiwa inaishi na Yesu. Mfano wa punje ya ngano unaelezea tumaini lililo ndani yetu sisi Masista: mbegu huoza ardhini na hatimaye huleta maisha mapya, matunda mapya.

Leo tupo hapa kwa ajili ya kusherehekea utakatifu wa Maria De Mattias pamoja na kuwaheshimu Masista 20, uwepo wao kama zawadi na Pasaka yao kuishi na Kristo. Na ni kwa shukrani kwa imani hii kwamba tunaweza kupokea kifo kama dalili ya furaha kubwa na inayofariji zaidi.

Imani tu ndiyo inayotupa uhakika kwamba hawa Masista wanaishi milele na sisi na kwamba wanatembea pamoja nasi. Kutenganishwa, ingawa inaweza kuwa chungu, ni kweli kunapunguzwa na ukweli kwamba siku moja tutajikuta katika nchi ya mbinguni na, kama Maria De Mattias alivyosema: mbele ya Mwanakondoo tutaimba utukufu wa Damu ya Kimungu. Na Mtakatifu Maria De Mattias tutasherehekea pamoja!

Kwa hiyo, maombolezo tuliyoyapata yamekuwa sala na shukrani. Tunataka kumrudishia Bwana baraka nyingi ambazo tumepokea kupitia Masista hawa: utume wao, huduma yao kwa maskini, kazi zao katika maeneo ya dharura, ya kutengwa, maisha yao waliyotumia kwa ajili ya Ufalme. Na tunataka kuwashukuru kwa kila kitu ambacho wamekifanya kwa uaminifu wao, kwa majitoleo yao. Lakini wakati huo huo tunataka kumwomba Bwana hekima ya kuelewa thamani ya maisha yetu, thamani ya vitu vidogo kama dhamana ya siku tulizo nazo, ili kusiwepo na kitu kinachopotea.



Kwa mantiki ya Injili, kwa mtindo wa Yesu, ambaye alimpenda hadi mwisho. Katika mwaka huu maalum sana, tunasherehekea kumbukumbu ya kutangazwa kwa Mtakatifu Maria De Mattias. Kwa mwangaza wa utakatifu wake, kuwakumbuka Masista hawa kunaturuhusu kushukuru baraka ya kile ambacho kimekuwa kwetu na kuwaacha waende kwa upendo na shukrani nyingi.

Katika sherehe hii, ambayo haikusudiwa kuwa sherehe ya mazishi lakini karamu, tunataka pia kuwa karibu na kila mmoja. Ndiyo sababu tulifikiria juu ya uhusiano huu, kuwa karibu, kama Mwili, na kusema shukrani zetu kwa Bwana kwa uaminifu wetu sisi sote katika wakati huu wa jaribu. Kwa ujasiri mkubwa wa mateso, ushuhuda wenye utulivu wa wengi wetu wenye maumivu, ujasiri licha ya kutokuwa na uhakika ambao umeonyesha maisha ya jumuiya zetu nyingi.

Katika Ekaristi hii tunaleta madhabahuni ishara nyingi za mshikamano, uwazi wa njia mpya za kushiriki na uchache ambao, katika sehemu nyingi za Shirika, wengi wenu Masista mmeendelea kuelezea. Alama nyingi za upendo, uwepo mwingi wa huruma, kila mahali kila mtu aliendelea kutumikia kwa gharama ya maisha yake mwenyewe.

Kwa hiyo, Ekaristi hii na iwe kweli fursa ya kuungana na Shirika zima, kwa kusali kwa kila Sista. Na kumshukuru Mungu kwa maisha ya kila Mwabudu, tukikabidhi matarajio yetu, wasi wasi wetu, na matumaini ya kila mmoja kwa Mtakatifu Maria De Mattias. Katika wakati huu wa kutokuwa na uhakika, uwepo wako wa kirafiki unatutia moyo kutazama siku zijazo kwa kuamini ahadi hiyo *kwa Mungu ambaye anafanya mambo yote kuwa mapya.*

Kila la heri kwangu, kwa kila mmoja wenu, popote mlipo.

***Sr Nadia Coppa, ASC***

# Toka Ulimwengu wa ASC

**Eneo la Bara: Ulaya**
**Region ya Italia**

## “Bwana Yesu, Unajifanya chakula na kinywaji kwa ajili yetu, ukituwekea Roho wako wa Kimungu ndani mwetu.”

*Utujalie tuweze kubadilishwa na Uwepo Wako hai tuweze kuitikia mwito wetu wa kushirikiana nawe katika fumbo la kazi yako ya ukombozi kwa wanadamu!*

*Heri*

Tulikuwa tukitamani sana kusherehekea tukio la Mtakatifu Maria De Mattias.

Hatimaye tarehe 18 Mei 2003, kwa furaha na shukrani, tukawa kwenye sherehe kuu huko Roma, kwenye uwanja wa Mtakatifu Petro uliokuwa umejaa watu kutoka sehemu mbali mbali za Ulimwengu, wakiwa na kofia nyekundu zilizokuwa zimeandikwa: “Thamani yako ni Damu ya Kristo”. Kwenye ukumbi mkubwa wa Kanisa kulikuwa na mchoro wa Maria De Mattia uliokuwa umechorwa na msanii Passeri di Priverno (LT), ilitawala shauku ya kimisionari, pamoja na watakatifu wengine watatu.

Ni hisia gani! Furaha iliyoje! Shukrani nyingi kwa Mungu kusikia Kanisa linatamka: Maria De Mattias Mtakatifu.

Baada ya miaka 18, shukrani kwa teknolojia, imetufanya tuweze kukumbuka siku nzuri ambayo mama yetu mwenye Heri alipotangazwa mtakatifu. Shukrani kwako Sr Nadia na uongozi wote kwa kuandaa mkutano maalum mkondoni na Shirika zima katika wakati huu wa janga. Tulifuata vizuri sana adhimisho la sherehe iliyofanyika katika Nyumba Kuu. Kuona kaburi la Mtakatifu wetu, Masista, washiriki mbali mbali, nyimbo na ngoma ya Masista na wapostulanti wa Kiafrika, ibada ya kuabudu ya Masista wa India, kilikuwa ni kitambulisho cha Uhai wa Shirika.

Asante mpendwa Mama Mkuu Sr. Nadia, salamu yako yenye utajiri wa kiroho, iliyotamkwa kw hisia za majonzi, ilitugusa moyoni. Pia, yalipotajwa majina ya Masista waliokufa kwa COVID-19, iliamsha hisia ya kila mtu. Kwa kweli, usafirishaji wa mawasiliano ulihitaji kazi, lakini haikuwa shida, kwa sababu tulichukua vizuri familia yetu ya kitawa, tulijiimarisha na hali ya kiroho, tukapata umiliki.

***Sr Sandria Latini, ASC***
***na Jumuiya ya Velletri***

iku maalum ya tarehe 18 Mei 2021



## Mimi shahidi wa upendo wa A.S.C

Mnamo tarehe 18 ° kumbu kumbu ya kutangazwa kwa Mtakatifu Maria De Mattias, Nilijawa na hisia na hamu kubwa moyoni na akilini mwangu, nikikumbuka nyakati zilizopita wakati tulipokuwa wasichana wadogo, tulipokwenda kwenye shule ya mapambo na A.S.C. (watawa)

Hizo zilikuwa nyakati zingine, lakini akina mama hao walikuwa wakaribishaji na wenye upendo sana kwamba sisi wasichana tupate kukimbilia kwao. Walimtii kikamilifu Mama Mwanzilishi ambaye alikuwa akirudia kwa kila mmoja wao *"ongea mara nyingi, zungumza na wasichana kwa moyo wa upendo usio na kipimo wa Mungu kwa kutupatia Mwanawe Mtakatifu zaidi, unazungumza pia juu ya uzuri mkubwa wa Yesu na Maria. Tumia njia zote nzuri kuwashawishi kwa wema; muwapende kwa upole, kwani wana thamani ya Damu Yesu na maumivu na uchungu kwa Bikira Maria "* (Mt.MdM)

Walikuwa wameunda kikundi cha "Preziosine" na Padri Michele Di Gioia walikuwa wakifundisha katekesi kila mwezi juu ya Damu ya Kristo na maisha ya Maria De Mattias.

Nyakati ninazoongelea ni ( kuanzia 1959 ) hizi ni nyakati ambazo "Masista wetu" walikuwa peke yao huko San Giovanni Rotondo na kwa hivyo kulikuwa na idadi kubwa ya waliojitokeza kwa shule ya awali na ile ya kudarizi.

Mwaka 2013, na Masista waliopo San Giovanni Rotondo, tulikuwa tumeanza tena shughuli hii, ambayo ni kuwafundisha wasichana sanaa ya ufundi wa kudarizi nguo na maisha ya Kikristo, lakini janga hilo lilitulazimisha kuacha. Nina imani kuwa hivi karibuni kila kitu kitaisha na tutaweza kurudi katika hali ya kawaida na kwa mwanzo wa mwaka wa shule, sisi pia, kwa msaada wa Bwana, tutaweza kuanza upya.

Hisia na upendo wangu wa dhati kwa "masista wetu" na Waabuduo wote wa Damu ya Kristo,

Mtakatifu Maria De Mattias utuombee kwa Mungu kwa ajili ya kupata miito mingi.

Sifa iwe katika Damu ya Kristo!

***Emilia Malerba, Mwalimu wa kudarizi,***
***San Giovanni Rotondo***

## Tafakari ya tarehe 18 Mei

Ulikuwa mkutano wa sala na hisia kubwa ambazo zilivuka mipaka ya kijiografia na kutufanya tujisikie karibu sana, hata katika umbali mkubwa sana.

Mtakatifu Maria De Mattias alikuwa akisema: " Kama kazi ni ya Mungu, hataacha kuibariki".

Iilikuwa ni jambo la kufurahisha kuona jinsi tamaduni mbali mbali zinavyoungana katika harambee ya kusifu thamani ya Damu ya Kristo kwa namna mbali mbali kimwili, kwa lugha na muziki ambao Roho Mtakatifu amempatia kila mtu uwezo wa kutafsiri kwa uelewano.

Shukrani hai kwa Bwana ambaye anaendelea kuibariki kazi iliyoanzishwa na Mtakatifu Maria De Mattias na Masista wote A.S.C. wa Uongozi Mkuu na wa Region ambao wamefunuliwa moyoni kuandaa wakati huu wa kukaa pamoja kwa kina na A.S.C. ambao wanafurahia maono makuu ya Mwanakondoo.


Idumu Damu ya Kristo!

***Rosalba Facecchia A.S.C***



Eneo la Bara: Ulaya
Region: Polonia





## Kumfuata Maria De Mattias

Tarehe 18 Mei 2021 tulisherehekea kumbu kumbu ya kutangazwa Mtakatifu Maria De Mattias, mtu ambaye alikutana na Yesu na alimpenda kwa moyo wake wote. Utunzaji wa kubadilishana upendo huu, kuufanya ukue na kuwa mpango wa maisha yake yote. Alitaka wengine wajue Upendo huu na wabaki katika maisha yao.

Maadhimisho ya kutangazwa kwake kuwa mtakatifu yanatukumbusha kuwa chanzo cha utakatifu wake hutoka katika Fumbo la Pasaka na anatualika kushiriki katika shule hii ya Upendo.

Nyakati ambazo tunaishi zimekuwa kwetu "masomo ya vitendo", majaribio ya maisha ya upendo na ubora wa uhusiano wetu na Mungu na watu. Tayari tumepata uzoefu wa umuhimu wao katika maisha yetu, na labda tunahisi njaa ya kukutana kibinafsi.

Ingawa bado hatuwezi kukutana kibinafsi, utumiaji wa viunganisho vya mtandao umeturuhusu kukutana kijumuiya kwa namna fulani, imetusaidia kukua kama mwili, na imetupa fursa ya kuwa na umoja katika Sala. Tulishukuru kwa zawadi ya maisha ya dada zetu waliokufa kutokana na Covid 19. Pamoja na shida za kiufundi, kukutana kupitia mtandao kulikuwa furaha yetu.

***Sr Ewa Piwonska, ASC***



Eneo la Bara: Ulaya
Region: Schaan

iku maalum ya tarehe 18 Mei 2021

# Mwangwi wa Sherehe

## SCHAAN

"SHUKRANI KWA JUHUDI ZENU ZOTE ZA KUWEZESHA SHEREHE YA EKARISTI IHUDHURIWE NA SHIRIKA ZIMA. ILIIMARISHA UHUSIANO KATI YA ASC WOTE NA KUTUJAZA FURAHA."

"TULIFUATILIA SHEREHE YA KUSISIMUA SANA KATIKA KIKANISA CHETU NA TULIWEZA KUPATA MAZINGIRA YA SALA. TULISALI NA KUIMBA PAMOJA NANYI NA PIA TULIWEZA KUPOKEA MWILI WA KRISTO ."

"UTAJIRI NA UZURI WA TAMADUNI MBALI MBALI ILIJIELEZEA PIA KATIKA KUANDAA MAADHIMISHO YA EKARISTI NA UKWELI UNAOWEZA KUELEWEKA, HASWA KATIKA MICHEZO NA NYIMBO."



"KILICHOTUGUSA ZAIDI NI KUMBUKUMBU YA WAHANGA ISHIRINI WA ASC WA JANGA LA COVID-19. PICHA ZAO NA MISHUMAA ILIYOWASHWA VIMEBAKI MIOYONI MWETU."

## ROTHENBACH

"ILIKUWA VIZURI KUPATA, KWENYE SKRINI NYINGI, MASISTA WENGI NINAOWAJUA NA WENGINE NILIKUWA SIJAWAONA KWA MUDA MREFU. FURAHA KUBWA ILIYOONYESHWA NA VIKUNDI ANUWAI VYA ASC BAADA YA SHEREHE HIYO ILIKUWA YA KUVUTIA KWELI."

"MCHANGANYIKO WA HAFLA MBILI MUHIMU, SIKU YA KUWEKWA WAKFU KWA MWANZILISHI WETU NA MAADHIMISHO YA DADA ZETU WALIOKUFA, ILIONEKANA KWANGU KITENDO KILICHOONGOZWA NA ROHO MTAKATIFU.

UTANGULIZI MREFU NA WA KINA WA SHEREHE ULISAIDIA KUELEWA MAANA NA KUTAZAMIA KWA MATUMAINI. KATIKA MAHUBIRI YAKE, KARDINALI JOAO BRAZ DE AVIZ ALIENDELEA KURUDIA MAWAZO YA SISTA NADIA, NA PIA NILIHISI HISIA KALI YA UNDUGU.

UBUNIFU ULIOONYESHWA KATIKA KUCHEZA, KATIKA NYIMBO, KATIKA ALAMA MBALI MBALI NI NGUVU YA JUMUIYA YETU KUBWA YA KIMATAIFA YA ASC. KUPITIA UNGANISHO LA ZOOM, SOTE TULIWEZA KUSHIRIKI NA KUSHEREHEKEA. MIMI, SISI KAMA JUMUIYA, TUNAWASHUKURU WOTE WALIOFANYA KAZI KWA AJILI YA SHEREHE HII."

Eneo la Bara: Ulaya
Region ya: Zagabria





"NILITARAJIA KUSHIRIKI KATIKA SHEREHE HIYO NA KWELI NIKAFANIKIWA. NIMEPITIA KATIKA JUMUIYA YETU YA KIMATAIFA, NIMEPATA MUUJIZA WA TEKNOLOJIA - AMBAYO INATUPA UWEZO WA KUUNGANA. HAFLA HIYO ILINIRUDISHA KANISANI AMBAPO, KWA MIAKA 13, KARIBU NA MWANZILISHI WETU MTAKATIFU, NILIMTUKUZA BWANA. WAKATI HUO HUO, ILINIKUMBUSHA SHEREHE YA KUTANGAZWA AMBAPO NILISHIRIKI. SHUKRANI KWA WALE WOTE AMBAO WAMEKUWA WAZI KWA ROHO MTAKATIFU, WALIKUBALI HATUA HIYO NA KUSHIRIKI KATIKA UTAMBUZI WAKE."

**Sr Blanka Šturm**

"ASANTE KWA WAZO NA MPANGO WA SHEREHE AMBAO UMEWEZA KUJUMUISHA MASISTA WENGI. ILIKUWA NI VIZURI KUONA SURA ZA MASISTA NINAOWAJUA, NA PIA SURA ZA WALE MASISTA AMBAO NIMEKUTANA NAO MARA MOJA TU, LAKINI AMBAO NINAWAKUMBUKA SANA. ASANTE KWA MAPIGO YA MOYO YALIYOTUFANYA KUGUNDUA TENA UZURI WA KUWA WA NASHIRIKA!"

**Hna. Marija Bilanović**

"KADIRI SHEREHE ILIVYOKUWA IKIENDELEA, NILIHISI KUUNGANA NA WAABUDU AMBAO WAKO MBINGUNI PAMOJA NA MTAKATIFU MARIA DE MATTIAS, NA SISI AMBAO BADO TUKO NJIANI. EKARISTI ILITULETA PAMOJA KUTOKA ULIMWENGUNI KOTE KATIKA MAOMBI NA IBADA YA MUNGU BABA MWENYEZI, IKIONYESHA DAMU YA YESU ILIYOMWAGIKA KWA UPATANISHO NA BARAKA. SHUKRANI KWA UONGOZI MKUU KWA WAZO NA MIPANGO AMBAYO ILITUWEZESHA SOTE TUKAWEZA KUWAPO, ANGALAU KWA MUDA, KATIKA JIJI LA MILELE LA ROMA - ISHARA NA KIINI CHA KANISA LA DUNIANI NA LA MBINGUNI."

**ASC Nova Topola**

## ZAGABRIA

"TULIIFUATIA SHEREHE HIYO KAMA JUMUIYA. TULIGUSWA NA SHEREHE HIYO, NA TULIHISI WASHIRIKI WENYE FURAHA WA SHIRIKA. TULIGUSWA NA SHEREHE HIYO, NA TULIHISI WASHIRIKI WENYE FURAHA WA USHARIKA. UZURI, MAELEWANO NA UTOFAUTI WA SHEREHE, UWEPO MAALUM WA MKUU. WAKATI WA KUSHANGAZA NA MZURI, KUWA WOTE WAPO MBELE YA SKRINI. NAOMBA MTAKATIFU WETU MARIA DE MATTIAS ATUOMBEE NA ATUPE WITO MPYA KUPITIA SHEREHE HIZI."

**ASC Razanac**



"ADHIMISHO LILIKUWA ZURI, MIPANGO ILIKUWA KATIKA KIWANGO CHA KUTUPELEKA KATIKA MWANGA WA UZURI WA UTOFAUTI KATIKA SHIRIKA."

**Sr Ancilla Vukoja**

Eneo la Bara: Ulaya
Region ya: Zagabria



"SHEREHE HIYO ILIKUWA YA KUGUSA NA YA HESHIMA. NILIHISI NGUVU YA DAMU YA KRISTO AMBAYO INAUNGANISHA UTOFAUTI WETU WOTE KUWA UMOJA MMOJA WA UMOJA. NI UTAJIRI MKUBWA WA KIROHO, UPENDELEO NA CHANZO CHA KUJIVUNIA KUWA ASC! NINAMSHUKURU MUNGU NA WOTE WALIOTOA TALANTA ZAO ILI KUUFANIKISHA WAKATI HUU WA KUGUSA NA WA KUMBUKUMBU YA KIROHO."

*Sr Benita Antolović*

"ILIKUWA NI VIZURI KUWA SEHEMU YA KUMBUKUMBU YA NYAKATI HIZO ZA KUFURAHIA. NILIHISI KWAMBA MTAKATIFU MARIA DE MATTIAS AMEINYOOSHA MIKONO YAKE JUU YETU, ALIKUWA AKIANGALIA NA KUFUATA MAISHA YETU NA SAFARI YETU YA KITUME."

*Sr Aneta Andelić*



## ZAGABRIA

"SHUKRANI KWA WAANDAAJI NA KWA URUSHAJI MZURI WA MISA TAKATIFU KWENYE KUMBUKUMBU YA KUTANGAZWA KWA MT. MARIA DE MATTIAS. ILIKUWA NI VIZURI KUSHIRIKI KATIKA SHEREHE HII PIA KUPITIA MTANDAO NA KUWAONA MASISTA WENGI KUTOKA ULIMWENGUNI KOTE. TUMWOMBE ILI KUPITIA MAOMBEZI YA MTAKATIFU MARIA DE MATTIAS, AFANYE UPYA SHIRIKA LETU KWA MIITO MIPYA. MTAKATIFU MARIA DE MATTIAS, UTUOMBEE."

*Hna. Stela Kovačević*

"SHEREHE YA MAADHIMISHO YA KUMI NA NANE YA UTAKATIFU WA MARIA DE MATTIAS ILIKUWA KWANGU USHUHUDA MZURI WA SHIRIKA LETU KATI YETU SISI WAABUDUO, AMBAO ULIKUWA NA NGUVU NA NEEMA MAALUM KATIKA NYAKATI HIZI NGUMU. UKARIBU WA MTAKATIFU MARIA DE MATTIAS NA MASISTA WETU WALIOKUFA HIVI KARIBUNI (WALIOWEKWA TAYARI KATIKA UWAKILISHI WA TONE LA DAMU) KATIKA SHEREHE HII ILIKUWA KITIA MOYO CHA KWELI KWANGU KUISHI WAKFU WA UBATIZO HATA ZAIDI KWA IMANI YA WAKATI HUU WA SASA. SHUKRANI KWA UONGOZI MKUU KWA WAZO HILI LA UBUNIFU."

*Sr David Dizdar*

**Eneo la Bara: Africa**
**Region: Tanzania**

## *Shukrani*

Tunamshukuru Mungu kwa siku hii ya leo tarehe 18/5/2021 tunapokumbuka siku ya Utakatifu wa Mama yetu Mtakatifu Maria De Mattias.

Tulifurahi sana tuliposhiriki katika adhimisho la Misa Takatifu tukisherehekea pamoja na Masista ASC Ulimwenguni pote kupitia online kwa lengo la KUWAOMBEA MASISTA 20 waliofariki kutokana na janga la Corona. Tunamshukuru Mungu kwa sadaka ya maisha yao walipokuwa wakishirikiana na Kristo katika kazi yake ya Ukombozi katika kumkomboa mwanadamu.

Muunganiko huu pamoja na salamu kutoka sehemu mbali mbali vilitupatia furaha ya pekee kwani tuliweza kuonana kupitia online.

Kushiriki kwetu katika Ibada hii ya Misa Takatifu kumetuwezesha kuonyesha Upendo na Shukrani kwa yale ambayo Masista wetu waliyafanya kwa ajili yetu sisi sote katika uhai wao.

Kwa namna ya pekee tunaushukuru Uongozi Mkuu kwa wazo hili Shirikishi na lenye kudumisha Upendo kati yetu kama ASC na kukua kama Mwili mmoja. Hizi ni shukrani zetu kwa niaba ya Jumuiya zote za ASC za Region yetu ya Tanzania ambazo zilishiriki katika adhimisho hili la pekee.



***Sr Coleta John, ASC***

**REGION TANZANIA**



iku maalum ya tarehe 18 Mei 2021

iku maalum ya tarehe 18 Mei 2021


# Mrejesho wa Sherehe

"NADHANI MKUTANO HUU ULIKUWA WA MUHIMU SANA AMBAO HAUJAWAHI KUTOKEA. ALISHUHUDIA KUWA SISI NI WAMOJA, LICHA YA MAENEO TOFAUTI YA KIJIOGRAFIA, LUGHA, KWAMBA SISI NI JUMUIYA CHINI YA USEMI WA KAWAIDA, ILE YA KUSHEREHEKEA MARIA DE MATTIAS NA MASISTA 20 WALIOKUFA KWA COVID KATIKA SHIRIKA LETU. KUANZIA WAKATI NYUSO ZA WATAWA ZILIPOANZA KUONEKANA KWENYE SKRINI, KILA MMOJA ALIHISI MHEMKO WA KUPENDEZA. WAABUDUO WALIFURAHI SANA KUPATA NYUSO ZA KIRAFIKI HIVI KWAMBA HAKUNA KITU KINACHOWEZA KUTUTENGANISHA. LITURJIA ILIYO NA NYIMBO NA NGOMA NA SIFA KATIKA LUGHA MBALI MBALI ILITHIBITISHA ROHO WA PEKEE ALIYETUZUNGUKA KATIKA KUKARIBISHA. ILIKUWA SHEREHE YA KABLA YA PENTEKOSTE. SHUKRANI ZA PEKEE KWA WALE AMBAO WALIFANYA KAZI KUWEZESHA MUUNGANIKO HUU WA EKARISTI NA ZOOM. NINAAMINI HUU UNAPASWA KUWA MWANZO WA MIKUTANO MINGINE KAMA HIYO."

*Sr Barb Smith, ASC Ruma Center*

**USA**





"ILIKUWA NI KAMA KURUDI MEI 18, 2003. HUDUMA NA UHUSIANO NA MTAKATIFU MARIA DE MATTIAS KATIKA SIKU YAKE MAALUM ILIKUWA NZURI. ILIKUWA VIZURI KUMWONA KILA MTU KWENYE ZOOM KATIKA SIKU YANGU YA KUZALIWA. ASANTE KWA KUTUPATIA NAFASI YA KUWAHESHIMU MASISTA WALIOKUFA KUTOKANA NA COVID-19. TULIMWOMBEA KILA MTU, MUZIKI ULIKUWA MZURI. UJUMBE KUTOKA KWA SR NADIA KATIKA SHEREHE HIYO PAMOJA NA WA MWADHIMISHAJI WA MISA ULIKUWA NI WA PEKEE. BARAKA KWETU SOTE."

*Sr Edwina Pope, ASC*

"NILIVUTIWA NA UMOJA AMBAO NILIHISI WAKATI WA SHEREHE. HATA INGAWA NILIKUWA MBALI NA MAELFU YA MAILI KUTOKA KWENYE SHEREHE HIYO, NILIHISI ROHO YA SHIRIKA LA WAABUDUO ULIMWENGUNI KOTE. ILIKUWA NI UKUMBUSHO WENYE NGUVU KWAMBA HAIJALISHI NI TOFAUTI GANI, TUMEUNGANA KATIKA WITO WETU NA MAJIBU YETU KWAKE."

*Sr Clare Boehmer, ASC*

"ILIKUWA NI FURAHA KUBWA NILIPOHUDHURIA MAADHIMISHO YA MISA KUPITIA ZOOM ... FURAHA HII NA SHAUKU ILIZIDI WAKATI NILIPOKUTANA NA ULIMWENGU WENYE TAMADUNI MBALI MBALI, KUUNGANISHWA KWA HAFLA HIYO. KUSIKIA MASISTA WA KIKROESHIA WAKIIMBA "NJOO KWENYE SHEREHE" ILIKUWA YA KUPENDEZA.

NDIO, WIMBO HUO ULIONEKANA KUKAMATA, IKIWA UTATAKA, UTAKATIFU, UKWELI WA WITO KWETU SISI SOTE: "MUNGU ATATOA, MUNGU ANASUBIRI KUKARIBISHA, KUSHIRIKI KIKOMBE ... KARAMU YANGU YA FURAHA ITAKULISHA ROHO NA IMANI NA UTIMILIFU WA MAISHA ".

KATIKA KRISTO, KUNA UMOJA, UMOJA NA JAMII ... SHEREHE YA EKARISTI ILIKUWA HALISI HAPA OFISINI KWANGU, UPANDE HUU WA BAHARI, KANA KWAMBA NILIKUWA KANISANI HUKO ROMA. SANTA MARIA DE MATTIAS, UNATUITA TENA KWA UMOJA HUO, KWA UPENDO NA MATUMAINI KATIKA DAMU YA THAMANI. ASANTE KWA WALE AMBAO WAMETUPATIA FURSA YA KUWAPO NANYI NYOTE KATIKA WAKATI HUU MWAFAKA."

***Sr Mary M. Shaw, ASC***

"NYUMBA YETU ILISHIRIKI.

KWANGU LILIKUWA NI JAMBO JEMA KUONANA NA KILA MSHIRIKI.

SHUKRANI KWA KUFANYIKA KWA TUKIO HILO."

***Hna. Joan Hornick, ASC***





iku maalum ya tarehe 18 Mei 2021

USA

Hisia zangu kutokana na sherehe:

Ilikuwa furaha kweli kweli kurudi kwenye sehemu yangu ya huduma, ambapo nilitumikia kwa miaka mitano! Kanisa ambalo tulisherehekea lilinikumbusha kumbukumbu nyingi, nyakati za sherehe, sala, machozi, kusikiliza, nk. Kwa kweli ni mahali pa neema! Kusherehekea na baadhi ya waabudu wale wale ambao nilisherehekea siku ya kutangazwa mwaka 2003 ni kumbukumbu ya "milele"!

Jumuiya ilikuwa imepang kutupeleka kwa Mtakatifu Petro siku hiyo, na pia tulileta na mmoja wa wanawake wazee ambao walisherehekea Ekaristi na sisi kila siku katika kanisa la Jenerali. Wakati dereva wa basi alipofungua mlango wa basi kwenye uwanja huo, kila mtu alikimbia kuchukua viti vilivyohifadhiwa mbele yetu. Nilielewa kuwa mwanamke huyu mzee hakuweza kukimbia, kwa hivyo nikasita nikabaki nyuma kutembea naye, nikijilaumu kwa sababu ya ubinafsi, kwamba hivi ndivyo Maria De Mattias angemfanyia mtu, kwamba nifurahi kufanya kile ambacho angefanya wamefanya, nk, nk, nk.

Wakati sisi wawili tulipofika, viti vyetu vya mbele vilikuwa na watu. Moyoni mwangu nilitaka kulia! Hakuna waabudu walikuwa pamoja nami kusherehekea siku hii muhimu sana, haswa kwa Waabudu! Wakati nikijionea huruma, nikatazama pande zote kuona watu wote wakija, bahari ya nyekundu kila mahali!

Nilimwona Elizabeth Muller wa Schaan akiongoza kikundi chake cha mahujaji, kwa hivyo nilimsalimia na kumuuliza ikiwa Sr. Zita Resch amekuja. Alisema ndio, alikuwepo mahali pengine kwenye umati. Mwishowe niligeuka na kule safu tatu tu mbele yangu, alikuwa Zita! Tulionana kwa wakati mmoja na tulifurahi! Mtakatifu Maria alijua kwamba nilihitaji kuwa karibu na mwabudu siku hiyo, na kulikuwa na rafiki hapo!


Kwa hiyo leo, miaka kumi na nane baadaye, huyu hapa Zita tena kwenye skrini ya Zoom na marafiki wengine wengi wa kuabudu ambao nilikuwa nimefanya huduma yangu nao: wanawake vijana (angalau mnamo 2001!) Ambao walishiriki kwenye semina ya malezi ya miezi mitatu na dada Wabrazil ambao walikuwepo, dada zangu huko Ufilipino ambao niliishi nao mnamo 2018, masahaba ambao niliishi nao katika Jenerali kutoka 2000 hadi 2005, na marafiki wengi, marafiki ambao katika nchi zao nilikuwa na bahati ya kwenda kutoa mafungo, wote kwenye Misa hii, kushiriki kiroho sawa na karama moja! Nilisikiliza kwa Kiitaliano kuona ni kiasi gani nilikumbuka baada ya miaka kumi na saba!

Ikiwa umoja ni zawadi nzuri, pia ni changamoto kubwa. Lakini lazima tukumbuke kuwa chochote kinachotupa changamoto kinaweza kutupatia ukuaji mpya. Dhamana yetu katika hali yetu ya kiroho na Karama yetu ni ya kudumu, ni kifungo cha kudumu! Asanteni kwa kutuwezesha sisi sote.

*Sr Mary Kevin, ASC*

Area Continentale: Asia
Regione India

## "Upendo usio na mipaka"



*"Wakati huruka na eneo hubadilika. Kuwa na imani kubwa na tumaini katika rehema ya Mungu, katika sifa za Yesu na kwa Damu yake." (St. MDM, # 874)*

Miaka kumi na minane imepita tangu kuwekwa wakfu kwa mwanzilishi wetu mpendwa Mtakatifu Maria De Mattias. Kila mwaka mnamo Mei 18 anatukumbusha maisha yake, aliishi kwa unyenyekevu kamili kwa mapenzi ya Mungu na kwa upendo wa kujitolea kwa ubinadamu. Mfano wake wa kishujaa, hata miaka 155 baada ya kifo chake, ni chanzo cha msukumo kwa kila mwabudu. Maneno yake "hata ikiwa niko mbali, siku zote niko karibu nawe kwa roho, binti yangu mpendwa; ndio, kwa upande wa Yesu Kristo, nakukumbatia kwa upole". (Mtakatifu MDM # 527) ni uthibitisho wa upendo wake na kuendelea kutuombea kwetu na kwa ulimwengu wote.

Huko India, Mtakatifu Maria De Mattias anapendwa na kukumbukwa na watu wengi. Kawaida, maadhimisho ya kutakaswa kwake huadhimishwa kwa njia nzuri na ya maana na maadhimisho ya jubilei au na taaluma ya kudumu ya Sista.

Lakini mwaka huu ilikuwa tofauti, kwani nchi nzima iko chini ya uangalizi wa karibu kwa sababu ya kuenea kwa ugonjwa huu. Habari za ukosefu wa vituo vya matibabu, viwango vya vifo visivyoweza kudhibitiwa, oveni zilizojaa kupita kiasi za moto na ving'ora vya gari la wagonjwa bila kuchoka vinaongeza hofu na kutokuwa na uhakika kwa siku zetu. Chini ya masharti haya, kuwa na chama au mkutano ni zaidi ya mawazo yetu.

Licha ya hali hizi mbaya, daima kuna mwangaza wa matumaini. Wakati hatukuweza kuwa na sherehe yoyote mwaka huu, wazo la kipekee na zuri la Uongozi Mkuu la kuandaa sherehe ya Ekaristi mkondoni lilithaminiwa sana na ishara ya ukaribu kwa kila mmoja wetu. Nina hakika kwamba, kama mimi, mamia ya Waabuduo waliokuwepo pia walisikia uchungu wa kuwapoteza dada zetu wapenzi wa ASC kutokana na Covid. Hapa kuna jukwaa ambalo limeundwa kuwa umoja kama familia moja, kwa nia moja na moyo mmoja, kuelezea mshikamano wetu wa pande zote, tukishiriki huzuni yetu kwa kuwapoteza dada zetu wapendwa. Wakati huo huo, ilikuwa fursa ya kukumbuka watu wengi waliopoteza uhai wao kwa sababu ya Coronavirus, kuwaombea pumziko la milele na kusema kwa heri na tumaini la Kikristo. Ninaamini kwamba ishara hii, daima hai na upendo na shukrani kwa dada zetu waliokufa, ambao kwa ajili yao hata hatukuweza kuwapa salamu ya mwisho, bado inaweza kumpendeza Mungu. Nina hakika kwamba kila mshumaa unaowaka kwa heshima yao hapa duniani pia itawashwa mbinguni, ikimuombea Mwanakondoo wa Mungu.



Uzoefu wa kukusanyika kama dada na marafiki karibu na meza ile ile ya Ekaristi kutoka maelfu ya kilomita ilinifanya nihisi kuwa sisi ni mwili mmoja, kwa hivyo tumeitwa kuwa umoja katika hali zote za maisha. Ilikuwa ni fursa kubwa kuwa na maoni ya sanduku la San MDM katika siku hiyo maalum. Mwadhama Kardinali João Bráz de Aviz ametupatia ladha ya karamu ya mbinguni kupitia sherehe nzuri na ya maana ya Ekaristi na ina alama ya kudumu akilini na moyoni mwa kila mwabudu. Mahubiri yake yaliuamsha tena usadikisho kwamba imani yetu tu kwa Mungu inaweza kutupa nguvu za kupitia nyakati hizi ngumu. Maneno yake yalikuwa ukumbusho kwetu sisi wote ambao, kama wanawake waliojitolea, tuna jukumu letu kuu kumfuata Yesu na kuwa na "upendo bila kipimo". Upendo huu usiopimika lazima uonyeshwe sio kwa Mungu tu, bali pia katika jumuiya zetu na kwa upande wote wa ubinadamu. Kutoka kwa maneno ya utangulizi ya Mkuu wa Shirika Sr. Nadia Coppa, niliweza kupata wasiwasi na upendo alio nao kama mama kwa kila mwanashirika. Moyo na macho yangu yalikuwa yamejaa kumsikiliza wakati akielezea shukrani kwa kila timu ya Region, kwa kila jumuiya na kwa kila Sista kwa huduma yao. Ujumbe wake ulinikumbusha kwa mara nyingine kuhesabu baraka za Mungu na kuweka maisha yangu kwenye kile ambacho ni muhimu kama mwanzilishi wetu. Natambua kuwa, kupitia maneno ya Sr Nadia Coppa, Mtakatifu Maria De Mattias alitukumbusha kuwa 'nafaka ya ngano iliyo tayari kufa ili kukamilisha hija yetu hapa duniani'. Zaidi ya yote, mpango huu mpya ulikuwa ishara ya upendo mkubwa na msaada kwa sisi sote na Uongozi Mkuu katika kipindi hiki cha janga. Kwa mara ya kwanza na kwa muda mrefu, ilitokea kwamba wengi wetu tuliweza kushiriki katika sherehe kwenye nyumba Kuu. Uzuri wa sherehe hii ni kwamba wakati tunapojiweka mbali na jumuiya na wanajumuiya na wengine, tunaweza kushikamana katika sala kiroho na Shirika lote. Ambapo ukaribu wa mwili haukuwezekana, tunaweza kuhisi nguvu na dhamana ya familia yetu ikiungana katika Damu ya Yesu. Kwa kweli, muonekano wa kanisa hilo, Waadhimishaji wa Misa, Masista wetu, Walei walinifanya nifurahi. Ninatoa shukrani zangu za dhati kwa adhimisho hili zuri wakati ambao kila mtu alikumbukwa na kila tamaduni iliwakilishwa. Ninatarajia kuwe tena na sherehe nyingine nzuri kwa pamoja katika siku zijazo. Kwa ujumla, ninahisi na ninaamini kuwa haikuwa tu maadhimisho ya utakatifu, lakini sherehe ya undugu wetu, mshikamano, uelewa na kuunga mkono. Kama binti za mtakatifu huyu mkuu, tunahitaji maombezi yake kwa uponyaji wa wanadamu wote, na kuishi wito wetu kama ishara ya matumaini na imani kwa kufuata mfano wake. Ni wakati wetu kuishi kitambulisho chetu cha Pasaka na kuomba nguvu ya Damu ya Kimungu kwa ulimwengu wote. Ninajiunga na ASC wote kwa roho, na ninamshukuru Sr. Nadia Coppa na Uongozi kwa kuifanya siku hii kuwa isiyosahaulika kwetu sote.



***Sr Chithra Pulikakkunnel ASC***

## Shukrani za Mkuu wa Shirika




*Shukrani fupi ambayo inatoka moyoni mwangu kwa uwepo wake, Mwadhama, ambaye aliufanya wakati huu kuwa muhimu sana.*

*Ni ishara inayoonekana ya mema ya Kanisa kwa maisha ya wakfu na kwa Shirika letu dogo. Ninakushukuru kwa sababu hakuna wakati wowote ukosefu wa ishara za umakini kwa Shirika na wakati wa kushiriki hekima yake ambayo wakati mwingine inanishirikisha. Hii inanisaidia katika huduma yangu, mimi ni kijana. Na ukiwa kijana unajichukua mwenyewe kila mahali ukitafuta nuru, unatafuta ujuzi, unatafuta neema. Na kwa hivyo nakushukuru kwa sababu uwepo wako pia ni ishara ya mema uliyonayo kwetu.*

*Kisha ninawashukuru kaka zetu. Namshukuru Padri Emanueli ambaye daima yuko makini, yuko kama kaka yetu. Namshukuru Padri Terenzio, Mkuu wa Kanda ya Italia. Padre Vito, rosminiani, hata wao daima wako makini pamoja nasi, na Padre Paolo, paroko wetu. Asante. Tumefurahishwa na uwepo wa Padre Stefano, Paroko wa Mtakatifu Caterina. Hii pia ni ishara ya uwepo wetu katika eneo hili. Uwepo ambao unabadilika kwa muda lakini, kama mbegu ndogo, hii inatufanya tuwe uwepo wa maombi, uwepo ambao unafanya kazi na unaenea ulimwenguni, kama vile Maria De Mattias alivyokuwa akiota kila wakati.*

*Tunawashukuru kaka zetu waseminari ambao wametusaidia kuandaa Liturjia. Nawashukuru Masista wote walioungana nasi, na hasa wale waliotafsiri. Kuna Masista ambao wameweza kutafsiri kwa Lugha mbali mbali za Shirika. Kwa hivyo, natumaini wote waliweza kuelewa uzuri wa kile tulichoweza kushiriki, ujuzi wa utajiri wa imani yetu.*

*Nataka kuwashukuru Wakuu wa Region ambao wameuwezesha wakati huu wakijaribu kuratibu vizuri hali hii ya dharura. Na ninawaita kwa majina kwa sababu wapo na ninataka kuwashukuru kutoka moyoni mwangu. Ninaenda kwa majina, na sio kadiri ya utaratibu wa umuhimu lakini kwa utaratibu wa kumbukumbu na kwa moyo:*

*Namshukuru Sr Ewa Kleps na na Masista wa Uongozi wa Region ya Polonia.*
*Sr Judith Kuman na Masista wa Uongozi wa Region ya Schaan.*
*Shukrani kwa Sr Lucina Johaness na Uongozi wa Region ya Tanzania.*
*Sr. Mini Palipadan na Uongozi wa Region ya India.*
*Shukrani kwa Sr Vicki Bergkamp na Uongozi wa Region ya US.*
*Sr Allessandra Soares Pereira na Uongozi wa Region ya Brasile.*
*Shukrani kwa Sr Zdravka Leutar na Uongozi wa Region ya Zagabria.*




*Shukrani za pekee zimwendee Sr. Nicla Spezzati, ambaye hayupo hapa, ambaye amewakilishwa na washauri kadhaa, namshukuru yeye, naushukuru Uongozi wa Region ya Italia, ambao wameguswa sana na tukio hili. Ninawashukuru kwa ushuhuda wao wa huduma, kujitolea, utunzaji wa hali nyingi za dharura ambazo zimelipuka, zote kwa pamoja, na ambazo zimegusa kweli maisha ya Region, ya Kanda ya Italia.*

*Shukrani kwa Sr. Lucia, Sr Giuseppina, Sr. Bruna, Sr Antonietta. Namshukuru pia Sr Milena, Sr. Miriam na kwa namna ya pekee, narudia, kwa Sr Nicla kwa huduma zao. Lakini pia kwa Msista waliopo kwenye jumuiya ulimwenguni kote, wamekuwa mstari wa mbele katika kuwatunza masista wakubwa. Tuna jumuiya nyingi za Masista walio katika mazingira magumu zaidi na kila mahali kumekuwa na umakini mkubwa, utunzaji mwingi wa hazina hizi za thamani ambazo ni Masista wakubwa. Kwa hivyo nakushukuru kwa dhati kwa upendo, utunzaji na umakini ambao tumepata katika wakati huu. Bwana atujalie tuweke hazina ili kugundua tena na kutunza asili ya Karama yetu. Tunahitaji kugundua upya uzuri wa Karama ambayo Maria De Mattias aliishi. Labda uzoefu huu ni ule ambao unatutakasa, unatusaidia kwenda kwenye mambo muhimu, natamani niwe mimi binafsi ninaihitaji lakini sisi sote tunahitaji kugundua nguvu hiyo ya Karama ambayo ni moto, ambayo ni shauku, ambayo ni mpya na huo ni uhai lakini sio kwa ajili yetu, bali kwa ulimwengu, kwa Kanisa na kwa wanadamu wote. Shukrani kwa wote. Shukrani kwa marafiki wengi waliojiunga nasi. Shukrani nyingi ziwafikie popote Ulimwenguni kwa fursa hii. Leo tumekuwa kweli mwili mmoja. Mimi najisikia niko karibu na Masista wote na ni ujuzi mzuri sana .*

*Asante kwa wote!*

***Sr Nadia Coppa, ASC – 18 mei 2021***

# Maadhimisho ya Vifo vya ASC vilivyotokana na COVID

| | | |
|---|---|---|
| 3 Novemba 2020 | **Josipa Santro** | Zagabria |
| 28 Novemba 2020 | **Elia Maurizia Di Salvo** | Italia |
| 2 Desemba 2020 | **Blandina Hug** | Schaan |
| 4 Desemba 2020 | **Elia Siddi** | Italia |
| 8 Desemba 2020 | **Elena Pannunzio** | Italia |
| 17 Machi 2021 | **Lucia Spadone** | Italia |
| 19 Machi 2021 | **Maria Carmela Tancredi** | Italia |
| 20 Machi 2021 | **Maria Zilda Moraes** | Manaus |
| 20 Machi 2021 | **Giovanna Valvano** | Italia |
| 22 Machi2021 | **Adele Massari** | Italia |
| 23 Machi 2021 | **Natalina Petrilli** | Italia |
| 24 Machi 2021 | **Teresa Dentico** | Italia |
| 28 Machi 2021 | **Rosaria Valente** | Italia |
| 30 Machi 2021 | **Antonietta Agherbino** | Italia |
| 1 Machi 2021 | **Concetta Mancini** | Italia |
| 2 Machi2021 | **Anna Maria Campanaro** | Italia |
| 2 Machi 2021 | **Antonietta Sangregorio** | Italia |
| 4 Machi 2021 | **Ester Manganiello** | Italia |
| 9 Machi 2021 | **Sabina Francone** | Italia |
| 16Machi 2021 | **Valeria Pilotti** | Italia |



## Siku maalum ya tarehe 18 Mei 2021

hafla ya maadhimisho ya miaka 18
**ya utakatifu Maria De Mattias**

**Gazeti la Kimataifa**
*Waabuduo Damu ya Kristo*

**Habiri ya kila mwezi**
*na*
***Waabuduo Damu ya Kristo***
***Mawasiliano ya Kimataifa - Uongozi Mkuu***
Via Maria De Mattias, 10 - 00183 ROMA
**Mwaka XXIII, 18 Mei 2021**

*Kamati ya wahariri*
**Maria Grazia Boccamazzo, ASC**
**Diana Filoni**

Tafsiri na

***Sr. Cecilija Milković*** - *Kikroeshia*
***Sr. Betty Adams*** - *Kiingereza*
***Sr. Anastazia Floriani*** - *Kiswahili*
***Sr. Bozena Hulisz*** - *Kipolishi*
***Sr. Miriam Ortiz*** - *Kihispania*
***Sr. Johanna Rubin*** - *Kijerumani*